

# HALMASHAURI YA WILAYA PANGANI

MKURUGENZI MTENDAJI  
HAL MASHAURI YA (W)  
PANGANI

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI AGOSTI, 2018

### UTANGULIZI

#### Mh Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri imepanga kutekeleza bajeti yake yenye jumla ya **Shilingi 14,607,518,752/-** zinazotarajiwa kukusanywa katika vyanzo mbalimbali ikiwemo makusanyo ya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu pamoja na ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani.

Kiasi hicho cha fedha pia kimepangwa kutumika kugharamia matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya watumishi, kugharamia miradi ya maendeleo katika maeneo yote ya wilaya ya Pangani na matumizi mengineyo.

### 1. MAPATO

#### Mh Mwenyekiti

Hadi Kufikia kipindi cha mwezi Agosti 2018 Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya shilingi **1,617,312,066/-** sawa na asilimia **11** ya makisio ya mwaka kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 1 linavyoonyesha hapa chini.

#### Jedwali Na. 1: Mapato ya Mwezi agosti, 2018

N a	CHANZO CHA MAPATO	MAKISIO MWAKA 2018/2019	JUMLA YA MAPATO JULAI 2018	JUMLA YA MAPATO AGOSTI 2018	JUMLA YA MAPATO JULAI HADI AGOSTI 2018	MAPATO PUNGUFU/ZAIDI	ASI LI MI A
1	Mapato ya ndani	1,341,553,996	41,895,728	27,207,970	69,103,698	(1,272,450,298)	5
2	Mishahara	10,546,936,000	677,655,000	664,952,000	1,342,607,000	(9,204,329,000)	13
3	Mapato ya ruzuku ya matumizi ya kawaida	1,732,340,253	0	60,821,508	60,821,508	(1,023,700,817)	6
4	Mapato ya ruzuku ya miradi	1,634,506,431	143,949,860	830,000	144,779,860	(1,489,726,571)	9
	<b>JUMLA</b>	<b>14,607,518,752</b>	<b>863,495,588</b>	<b>753,811,478</b>	<b>1,617,312,066</b>	<b>(12,990,206,686)</b>	<b>11</b>

## 2. MATUMIZI

Mh Mwenyekiti,

Hadi kufikia mwezi Agosti, 2018 jumla ya Shilingi **1,513,531,000/=** zimetumika na kufanya matumizi kufikia asilimia **10.36** ya makisio ya mwaka, na zimetumika katika vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 2 linavyoonyesha hapa chini.

### Jedwali Na. 2: Matumizi Mwezi Agosti, 2018

N A	CHANZO CHA MATUMIZI	MAKISIO MWAKA 2018/2019	JUMLA YA MATUMIZI JULAI 2018	JUMLA YA MATUMIZI AGOSTI 2018	JUMLA YA MATUMIZI JULAI HADI AGOSTI 2018	MATUMIZI PUNGUFU/ZAIDI	ASILIMIA
1	Mapato ya ndani	1,341,553,996	0	44,282,000	44,282,000	1,297,271,998	5.59
2	Mishahara	10,546,936,000	677,655,000	664,952,000	1,322,607,000	9,901,984,000	12.54
3	Mapato ya ruzuku ya kawaida	1,732,340,253	0	1,560,000	1,560,000	1,082,962,325	0.14
4	Fedha za miradi	1,634,506,431	0	145,082,000	145,082,000	1,489,424,431	8.88
	<b>JUMLA</b>	<b>14,607,518,752</b>	<b>677,655,000</b>	<b>835,876,000</b>	<b>1,513,531,000</b>	<b>13,771,642,754</b>	<b>10.36</b>

## MAFANIKIO

Mh Mwenyekiti,

Makusanyo ya vyanzo vya ndani pekee ni jumla ya **Shilingi 27,207,970/=** sawa na **asilimia 5**.

## MAFANIKIO

Mh. Mwenyekiti

- Tumefanikiwa kupata maridhiano ya ushuru mpya wa vibanda vinavyozunguka stendi na soko. Hivyo tumeabdaa mikataba mipya na utekelezaji unaendelea.
- Tumefanikiwa kuwapatia watendaji mashine tano za kukusanyia mapato (POS)

## **CHANGAMOTO**

### **Mh Mwenyekiti**

- ✓ Kutozingatiwa kwa sheria ndogondogo kwa ushuru wa Mazao ya chakula na misitu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kunapelekea kupungua kwa mapato.
- ✓ Mabadiliko ya hali ya hewa kwa mwezi julai yamepelekea mapato ya ndani kupungua hasa katika ushuru unaotokana na mazao ya bahari.

## **MIKAKATI**

### **Mh mwenyekiti**

- Kuendelea kutoa elimu ya tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda vidogo na vikubwa.
- Kuendelea kuboresha sheria ndogo kila panapohitajika kufanya hivyo ili ziendane na wakati.
- Kusimamia wakusanyaji wetu ili ukusanyaji wetu uwe na tija kwa pande zote mbili. Ikiwemo kusimamia mapato yote kwa kufanya doria na kuendelea kutoa asilimia 20 zao kwa wakati.

MKURUGENZI MTENDAJI  
HAL MASHAURI YA (W)  
PANGANI